



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA



Unapojibu tafadhali taja:
Kumb Na.EB.89286/-2A/105

08/01/2025

TANGAZO LA NAFASI (02) ZA KAZI ZA MKATABA - DEREVA II

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa nafasi **mbili (02)** za Kazi za Mkataba Dereva II.

SIFA ZA MWOMBAJI:

Mwenye cheti cha kidato cha Nne (Form Four) na leseni Daraja C au E ya uendeshaji magari ambaye amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU YA DEREVA II:

- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- vi. Kufanya usafi wa gari; na
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri utakavyoelekezwa na Msimamizi wako

NGAZI YA MSHAHARA:

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya serikali yaani **TGS B/1**

MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI:

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45 isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini;
- ii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (Detail C.V) yaliyojitosheleza (Detail Curriculum Vitae) yenye anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na Anuani ya Barua Pepe (E-mail address), majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na kitambulisho cha Taifa (namba ya kitambulisho cha Taifa).
- iii. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia Sifa za kuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitische barua zao za maombi yanafasi ya kazi kwa waajiri wao na waajiri wao wajiridhishe ipasavyo.
- iv. Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne au Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya Udereva.
- v. Testmonial“, “Provisional Results“, “Statement of results“, hati ya matokeo ya Kidato cha Nne na Kidato cha Sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**
- vi. Waombaji waliosoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na vimethibitishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).
- vii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.
- viii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.
- ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

x. Maombi yote yatumwe kupitia anuani ifuatayo;

**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Ngara,
S.L.P 30,
NGARA.**

xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **21 Januari, 2025.**

MUHIMU: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe hapo juu.

KUMBUKA: Maombi yatakayo wasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili. **HAYATAFIKIRIWA.**

Imetolewa na;


Emanuel P. Kulwa
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NGARA